**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MAGU**
(Barua zote zipelekwe kwa Mkurugenzi Mtendaji Wilaya)

**MKOA WA MWANZA**
Simu:- 028 – 2530002
FaxNo.:-028 – 2530199
Kumb. Na. MDC/S.10/160/97

Sanduku la Posta 200
**MAGU.**

31.07.2018

# TANGAZO LA AJIRA YA KAZI KWA MKATABA

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Magu kwa kushirikiana na Shirika la AGPAHI anawatangazia nafasi za Ajira kwa Mkataba wa miezi 3 mitatu katika fani mbali mbali kwenye vituo vya kutolea tiba Wilayani Magu. Mkataba unaweza kuongezwa kulingana na uwezo wa mhusika.

## 1.1: DAKTARI DARAJA LA II (MEDICAL DOCTOR II) NAFASI 2

**Sifa za kuajiriwa:**
Kuajiriwa wenye shahada ya udaktari kutoka chuo kikuu kinachotambuliwa na serikali waliohitimu mafunzo ya mazoezi katika kazi (internship) yaliyoidhinishwa na Baraza la madaktari Tanganyika (Medical Council of Tanganyika) na kusajiliwa kisheria na baraza hilo.

**KAZI NA MAJUKUMU:**

- Kufanya shughuli zote za matibabu Hospitalini zinazohusiana na magonjwa ya kawaida, magonjwa ya watoto, magojwa ya akina mama na upasuaji wa kawaida na dharula
- Kufanya kazi zote za kinga na afya ya jamii na kubuni mkakati ya kupambana na magonjwa yanayoambukiza
- Kusimamia watumishi wodini na sehemu zingine za kazi
- Kutoa ushauri nasaha kwa wagonjwa na jamii kwa ujumla
- Kufundisha na kuwaendeleza kitaaluma watumishi walioko kwenye hospital.
- Kufanya utafiti kuhusu magonjwa na kueneza matokeo ya utafiti kwa jamii
- Kupanga, kufatilia na kutathimini utoaji wa huduma za afya
- Kazi zingine atakazo pangiwa na mkuu wake wa kazi

**Kiwango Cha Mshahara Tsh. 1,500,000= kwa mwezi**

**1.2: MUUGUZI DARAJA II (NURSE II) - NAFASI 6**

Kuajiriwa wahitimu wa kidato cha nne (F IV) waliofuzu mafunzo ya uuguzi katika chuo kinachotambuliwa na Baraza la wauguzi na wakunga Tanzania au mafunzo ya uuguzi katika ngazi ya cheti na wenye uzoefu wa kazi kwa muda usiopungua miaka mitatu.

**KAZI NA MAJUKUMU:**

- Kutoa huduma ya ki-uuguzi kwa wagonjwa/wateja kwa kuzingatia sheria, maadili ya taaluma pamoja na miongozo iliyopo katika sehemu za kufanya kazi
- Kutoa elimu ya afya kwa wagonjwa/jamii
- Kufuatilia matatizo ya kiafya ya wagonjwa na jamii katika mazingira yao
- Kutoa huduma za chanjo kwa mama na mtoto na uzazi salama
- Kusimamia, kuratibu na kufuatilia kazi za walio chini yake
- Kufanya kazi nyingine kama atakavyopangiwa na mkuu wake wa kazi
- Anaweza kupangiwa kufanya kazi katika zahanati, kituo cha afya na hospitali ya Wilaya

**Kiwango cha mshahara – Tshs. 600,000= kwa mwezi**

**1.3: MTEKNOLOJIA WA MAABARA - NAFASI 1**

Kuajiriwa wahitimu wa kidato cha nne/sita wenye stashahada ya kawaida katika jamii ya maabara (Laboratory Technology).

**KAZI NA MAJUKUMU:**

- Kupima sampuli ili kutambua magonjwa
- Kutengeneza dawa za kufanyia vipimo vya maabara
- Kuhifadhi sampuli mbalimbali zinazotakiwa kufanyiwa uchunguzi au kupelekwa maabara za ngazi za juu
- Kuweka kumbukumbu za maabara ambazo zimepatikana wakati wa uchunguzi
- Kufundisha watumishi walio chini yake
- Kutunza vifaa vya maabara
- Anaweza kufanya kazi katika hospitali ya Wilaya na vituo vya afya

**Kiwango cha mshahara Tshs. 600,000= kwa mwezi**

**1.4: Data Clerk - Nafasi – 1**

**Sifa za kuajiriwa**

- Stashahada ya Juu au Shahada ya IT, Takwimu au utunzaji wa kumbukumbu kwa njia ya kielektroniki (EMR)
- Awe na uzoefu wa mwaka 1 – 3 katika kazi za Takwimu (Data Management)
- Awe na uzoefu na takwimu za afya (Health Data Experience)
- Awe na uzoefu wa kutumia mifumo ya DHIS2, Ms Excel, Ms Access, EPI – Info, SPSS na uzoefu wa mifumo mingine itakuwa ni sifa ya nyongeza

**Lengo la Ajira:**

Ni kuhakikisha Mfumo wa $CTC_2$ Data Base unafanya kazi kwa usahihi ikiwa ni pamoja na ubora wa Takwimu,

- Utunzaji wa mfumo $CTC_2$ Data Base
- Kuhuisha $CTC_2$ Data Base
- Kuingiza takwimu za wagonjwa kila siku na kutengeneza taarifa na kuziwasilisha katika ngazi husika

**Majukumu Makuu:**

- Kurudisha faili za wagonjwa ambao hazijajazwa vizuri kwa Mganga (Clinical ili zirekebishwe)
- Kufuatilia takwimu zilizopo kwenye $CTC_2$ Data Base zilizoingizwa ki-makosa na kuzirekebisha
- Kuhakikisha kila file la mgonjwa linakuwa na fomu za kuchunguza ugonjwa wa kifua kikuu (TB Screening tool) na magonjwa na ngono STI (Screening tool) na kuhakikishwa zinajazwa na Mganga kila mgonjwa anapohudhuria Kliniki
- Kuhakikisha takwimu zilizopo kwenye $CTC_2$ Data Base kila siku zinaingizwa (Data Cleaning)
- Kutengeneza mpango kazi wa kuboresha takwimu katika kituo husika katika mfumo wa $CTC_2$ Data Base na katika vyanzo vya Takwimu (Data Source)
- Kuhakikisha matumizi sahihi ya mfumo unafanya kazi kila wakati, kuhuisha antivirus kila siku
- Kuhakikisha unawasiliana na viongozi wako kwa wakati kwa ajili ya ukarabati wa mfumo pindi tatizo linapotokea.
- **Kiwango cha mshahara Tshs. 510,000/= kwa mwezi**

**MASHARTI YA UJUMLA:**

Waombaji wote wanatakiwa kuwasilisha barua zao kwa mkurugenzi wakiambatisha nakala ya

- Vyeti vya shule, taaluma na usajili
- Picha mbili ndogo za hivi karibuni
- Wasifu wa mwombaji (CV)
- Mwombaji aandike namba za simu
- Barua zote ziandaliwe kwa mkono.

**AJIRA**

Mwombaji ataajiriwa kwa mkataba wa miezi mitatu (miezi 3) muda ukiisha anaweza kuongezewa muda kulingana na utendaji kazi wake na Shirika la AGPAHI, hadi mradi utakapofika mwisho mwaka 2020.

Maombi yatapokelewa hadi tarehe **10/08/2018** saa **9.30 mchana,** muda wa saa za kazi

Maombi yatumwe kwa,

**Mkurugenzi Mtendaji (W)**
**Halmashauri ya Wilaya ya Magu**
**S.L.P. 200,**
**Magu.**

Imetolewa na

Lutengano G. Mwalwiba,
**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
MAGU.